

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 52 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JUNI 2025

MWENYEITI TSC AKEMEA WATUMISHI WANAOSAMBAZA TAARIFA ZA SERIKALI KINYUME NA TARATIBU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akifunga awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TSC YAS Aidie Tume Kuendelea Kuwa Chombo Imara Cha Kutenda Haki

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendesha mafunzo kwa watumishi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa Utumishi na Maadili ya Walimu nchini.


Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa awamu mbalimbali yaliwahusisha Makamishna wa Tume, Maafisa kutoka Tume Makao Makuu na Ofisi za Wilaya, Watumishi wa Kada Saidizi kutoka Ofisi zote za Tume na sasa mafunzo hayo yanatolewa kwa wajumbe wa Kamati za Wilaya ambao walikuwa hawajafikiwa.

Kwa ujumla tunaweza kusema mafunzo

hayo yamemgusa kila mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu na yamesaidia kutoa uelewa mpana zaidi kuhusu usimamizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za Walimu.

Imani yetu ni kuwa kutokana na juhudi hizo ambazo ni za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi hodari wa Rais Samia Suluhu Hassan, kila mtumishi wa Tume bila kujali nafasi aliyonayo ana wajibu wa kuhakikisha Tume inaendelea kuwa chombo imara kinachozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu na hivyo kuhakikisha haki inatendeka.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



MWENYEITI TSC AKEMEA WATUMISHI WANAOSAMBAZA TAARIFA ZA SERIKALI KINYUME NA TARATIBU

Na Mwandishi Wetu – Tabora.

Mwenyeiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke amekemea tabia ya baadhi ya watumishi wa umma wakiwemo walimu ya kusambaza taarifa za serikali kwenye mitandao ya kijamii jambo ambalo ni kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Hivyo, amewaagiza watumishi wa TSC kutoa elimu kwa walimu juu ya umuhimu wa kutunza siri za ofisi pamoja na madhara yanayoweza kutokea kwa mtumishi kwa usambazaji wa taarifa kwenye mitandao ya kijamii kinyume na taratibu.

Prof. Muruke ameyasema hayo tarehe 29 Mei, 2025 wakati akifunga awamu ya tano ya mafunzo kwa Watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi yaliyofanyika kwa siku nne kuanzia tarehe 26 – 29 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Kampasi ya Tabora.

“Siku hizi tunaona mambo mengi ya ofisi yanarushwa kwenye mitandao. Mimi nimesikia kuna barua za walimu zipo kwenye mitandao, nikajiuliza ni nani kapeleka? Lakini inawezekana ni wao wenyewe kwa sababu hawana uelewa wa kutosha kuwa moja ya mambo ya msingi katika maadili ya utumishi wa umma ni pamoja na kutunza siri za ofisi.”

“Hivyo, baada ya mafunzo haya mnapaswa kwenda kuwaelimisha walimu wetu kuhusu umuhimu wa kuwa wazalendo, kutotumia mitandao ya kijamii kusambaza taarifa za ofisi pamoja na madhara yanayoweza kumpata mwalimu kwa kukiuka taratibu za kutoa taarifa za Serikali,” alisema.

Moja ya mambo yaliyofundishwa katika mafunzo hayo ni menejimenti ya utambuzi wa hisia katika kusimamia uendeshaji wa mashauri ya nidhamu ambapo Prof. Muruke alisema mada hiyo ilitolewa ili kusaidia watumishi wa Tume kutumia ubinadamu katika kuwahudumia walimu.



Mwenyeiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akifunga awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

“Wakati wa kufanya kazi zetu tuwe binadamu, tukumbuke kwamba walimu wanaoletwa mbele yetu nao ni binadamu, ni wafanyakazi na wanapitia changamoto nyingi. Hivyo, tunapaswa kuwa sehemu ya kuwasaidia ili wawe watumishi wenye maadili badala ya kila wakati kufikiria kuwafukuza kazi,” alisema.

Aidha, kiongozi huyo alisema kuwa watumishi wa Tume wanapaswa kuwa na maadili ili wawe mfano wa kuigwa kwani wao ndio wanaosimamia nidhamu ya walimu huku akifafanua kuwa mtumishi asiye kuwa na nidhamu hawezi kusimamia nidhamu kwa wengine.

Awali, akitoa neno lakumkaribisha Mwenyeiti huyo, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa baada ya awamu ya tano ya mafunzo hayo kukamilika watumishi wote wa TSC ikijumuisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi watakuwa wamepatiwa mafunzo..

Alisema kuwa wazo la kutoa mafunzo hayo kwa watumishi wote wa Tume lilitokana na kuwepo kwa changamoto ambazo ziliibua malalamiko kutoka kwa walimu

hususan katika uendeshaji wa mashauri ya nidhamu.

“Changamoto ya kwanza ilikuwa ni ucheleweshwaji wa haki kutokana na ucheleweshaji wa mashauri ya nidhamu. Jambo lingine ilikuwa pale ambapo masuala ya mashauri yanachakwatwa lakini hayafiki mwisho au yanafika mwisho lakini siyo kwa ufasaha,” alisema.

Aliongeza kuwa, “Kwa hiyo hizi changamoto kuu mbili na uelewa ambao ulikuwa hafifu kwa watumishi wa Tume, ilionekana kuwa ni vyema watumishi wote wapate mafunzo kwa lengo la kuwawezesha kupata uelewa wa utekelezaji wa majukumu yao, lakini pia kupata miongozo ambayo wataitumia kama rejea katika majukumu yao ya kazi.”

Katibu huyo alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa watumishi kujengewa uwezo na kutoa maelekezo kwa Tume kutekeleza jambo hilo ambapo alieleza kuwa kwa upande wa watumishi wa Tume agizo hilo limetekelewa kwa asilimia 100 kwa kuwa watumishi wote wamepatiwa mafunzo.

MWENYEITI TSC AKEMEA WATUMISHI WANAOSAMBAZA TAARIFA ZA SERIKALI KINYUME NA TARATIBU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga arwamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Bw. Peter Bunyazu akitoa utambulisho wakati wa kufunga arwamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye hafla ya kufunga arwamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

MWENYEITI TSC AKEMEA WATUMISHI WANAOSAMBAZA TAARIFA ZA SERIKALI KINYUME NA TARATIBU



Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye hafla ya kufunga awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa vyeti kwa washiriki wa mafunzo ya siku nne ya yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi wa TSC tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

**MWENYEITI TSC AKEMEA WATUMISHI WANAOSAMBAZA
TAARIFA ZA SERIKALI KINYUME NA TARATIBU**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa vyeti kwa washiriki wa mafunzo ya siku nne ya yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi wa TSC tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

MWENYEITI TSC AKEMEA WATUMISHI WANAOSAMBAZA TAARIFA ZA SERIKALI KINYUME NA TARATIBU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na washiriki wa mafunzo ya watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 29 Mei, 2025 mkoani Tabora.

PRO. MURUKE AWATAKA WATUMISHI TSC KUONGEZA NGUVU KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKWAJI WA MAADILI

Na Mwandishi wetu –
Dar es Salaam.

Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wametakiwa kufanya juhudi katika kutoa elimu kwa walimu ili kuwaepusha kukiuka maadili ya kazi ya ualimu wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke wakati akifungua mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume hiyo.

Alieleza kuwa lengo la TSC ni kuhakikisha walimu wanatekeleza majukumu yao ya kufundisha wanafunzi kwa kuzingatia maadili ya kazi hiyo, hivyo aliwataka maafisa hao kujikita katika kuzuia ukiukaji wa maadili kwa kutoa elimu badala ya kusubiri wakosee ili wawachukulie hatua za kinidhamu.

Alisema kuwa kuwepo kwa mashauri mengi ya nidhamu siyo sifa njema ya kuonesha kuwa ofisi inatekeleza majukumu yake ipasavyo bali kazi inayohitajika ni kuhakikisha kuwa kila mwalimu anazingatia sheria, kanuni na taratibu na hivyo hakuna mashauri yanayojitokeza.

“Sio sifa nzuri kufukuza kazi walimu bali ni muhimu kutoa elimu kwa kuwatembelea mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wa kujua Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma na kuzingatia katika utendaji wao wa kazi,” alisisitiza.

Pamoja na hayo, Prof. Muruke alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa maafisa wa Tume kwani yatawajengea uelewa katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu na hivyo kuwezesha kuzingatiwa kwa misingi ya haki katika kutoa uamuzi.

Kwa upande wake Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akifungua mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.

Paulina Nkwama alisema kuwa chimbuko la mafunzo hayo ni kuondoa dosari za kutozingatiwa kikamilifu kwa taratibu wakati wa kushughulikia mashauri nidhamu jambo linalosababisha rufaa za walimu zinazokatwa Tume Makao Makuu kurudishwa ili mashauri yaanzishwe upya kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Aliongeza kuwa rufaa kurudishwa ili mashauri yaanzishwe upya siyo tu kwamba inasababisha kucheleweshwa kwa haki bali inasababishia hasara Serikali, hivyo aliwataka washiriki hao kuzingatia mafunzo ili watakaporudi kwenye vituo vyao vya kazi waongeze ufanisi wa utendaji kazi.

“Matarajio yetu ni kwamba baada ya mafunzo haya mtakwenda kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi. Tunatarajia kwamba hakuna rufaa itakayorudishwa ili shauri lianzishwe upya kwa kuwa taratibu hazikuzingatiwa,” alisema Mwl. Nkwama.

Katika hatua nyingine, Katibu huyo alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi

zake anazofanya katika kuboresha sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kuwezesha watumishi wa Tume kupata mafunzo hayo muhimu.

Awali, akitoa neno la utangulizi Mkuu wa Chuo na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Dkt. Ernest Francis Mabonesho alisema kuwa uhai wa taifa unategemea watumishi wenye weledi na mtazamo chanya kwa Serikali yao.

Alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwani yatawawezesha kuwa na uelewa wa kutosha katika kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu na hivyo kusaidia sekta ya elimu kuendelea kupiga hatua kimaendeleo.

Mafunzo hayo yanayoendeshwa chini ya ufadhili wa Programu ya kuboresha kada ya ualimu (GPE TSP) na kuendeshwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania yamewahusisha Maafisa wa TSC Makao Makuu na wengine kutoka Ofisi za Wilaya za Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Morogoro, Songwe na Iringa.

PRO. MURUKE AWATAKA WATUMISHI TSC KUONGEZA NGUVU KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKWAJI WA MAADILI



Mkuu wa Chuo na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Dkt. Ernest Francis Mabonesho akitoa salamu za Chuo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akifungua mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.



Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Aggrey Mleli (kulia), Mariam Haji (katikati) pamoja na Meneja wa Kituo cha Mafunzo Dar es Salaam wa Tume ya Utumishi wa Umma Tanzania, bi Zena Hussein (kushoto) wakiwa kwenye ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.



Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi nidhamu na rufaa za walimu yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.

PRO. MURUKE AWATAKA WATUMISHI TSC KUONGEZA NGUVU KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKWAJI WA MAADILI



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke (katikati) akiwa katika picha pamoja na viongozi na washiriki wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu yaliyowahusisha watumishi wa TSC tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.



Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi nidhamu na rufaa za walimu yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 5 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam.

Mafunzo ya usimamizi wa nidhamu na rufaa za walimu kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu yakiwa yanaendelea katika madarasa ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.

PRO. MURUKE AWATAKA WATUMISHI TSC KUONGEZA NGUVU KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKWAJI WA MAADILI



Mafunzo ya usimamizi wa nidhamu na rufaa za walimu kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu yakizwa yanaendelea katika madarasa ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.

MAKAMISHNA TSC WATEMBELEA UJENZI WA OFISI ZA TSC MAKAO MAKUU, WATAKA KASI YA UJENZI IONGEZEKE



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa kwanza kulia) akizungumza wakati wa ziara ya Makamishna wa Tume kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma iliyofanyika tarehe 12 Mei, 2025.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Masoud Hadi Muruke wamemtaka Mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu kuongeza kasi ya utendaji kazi ili jengo hilo likamilike kwa haraka.

Agizo hilo lilitolewa tarehe 12 Mei, 2025 wakati Makamishna wa Tume walipotembelea ujenzi huo unaofanyika katika kiwanja namba 77, kitalu BB eneo la uwekezaji Njedengwa jijini Dodoma.

Viongozi hao walionesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi huo ambao umefikia asilimia 57 huku muda wa kumalizika kwa mkataba ukiwa ni chini ya mwezi mmoja.

Akitoa maelezo ya awali kwa Makamishna wa Tume, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa Tume inaendelea na usimamizi wa ujenzi wa jengo la Ofisi lenye

ghorofa tatu ambalo linajengwa na Mkandarasi SUMA JKT Kanda ya



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa kwanza kulia) akionesha jambo wakati wa ziara ya Makamishna wa Tume kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma iliyofanyika tarehe 12 Mei, 2025.

Kati ambapo Mkataba wa awali wa kutekeleza mradi huo ulikuwa wa miezi 18.

“Tarehe ya awali ya kukamilika kwa ujenzi kwa mujibu wa mkataba ilikuwa Juni 5, 2024. Baada ya muda wa nyongeza mradi huo unatarajiwa kukamilishwa Juni 5, 2025,” alisema Mwl. Nkwama.

Akizungumza kwa upande wa Mkandarasi SUMA JKT, Major S. S. Jambo alisema kazi ambazo zimekamilika ni pamoja na ujenzi wa ukuta (walling) kwenye ghorofa ya chini na ya kwanza, kupiga ripu (Plastering) kwenye baadhi ya maeneo yaliyojengwa ukuta na kumwaga roof beam ikiwa ni matayarisho kwa ajili ya kuezeka baada ya ghorofa ya tatu (3) kukamilika.

Major Jambo aliahidi kuongeza kasi ya utendaji kazi kuhakikisha mradi huo unakamilika ili Tume iweze kutekeleza majukumu yake katika mazingira bora zaidi.

MAKAMISHNA TSC WATEMBELEA UJENZI WA OFISI ZA TSC MAKAO MAKUU, WATAKA KASI YA UJENZI IONGEZEKE



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kulia) akizungumza wakati wa ziara ya Makamishna wa Tume kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma iliyofanyika tarehe 12 Mei, 2025.



Ziara ya Makamishna wa Tume kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma tarehe 12 Mei, 2025 ikiwa inaendelea.

Major S. S. Jambo kutoka SUMA JKT akitoa maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu wakati wa ziara ya Makamishna wa Tume kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma iliyofanyika tarehe 12 Mei, 2025.

TSC BIHARAMULO YAENDESHA MAFUNZO KWA WALIMU WA AJIRA MPYA

Na Mwandishi Wetu – Biharamulo.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Biharamulo tarehe 24 Mei, 2025 iliendesha mafunzo elekezi kwa walimu 76 wa Shule za Sekondari walioajiriwa kwa kipindi cha Februari hadi Machi 2025 katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa lengo la kuwajengea uwezo juu ya taratibu mbalimbali zinazosimamia Utumishi wa Walimu.



Picha ya pamoja kati ya Kaimu Katibu Msadidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Biharamulo (tisheti ya bluu) na washiriki wa mafunzo elekezi kwa walimu wa Shule za Sekondari walioajiriwa kwa kipindi cha Februari hadi Machi 2025 katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 24 Mei, 2025.

TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSIMAMIA UTUMISHI NA MAADILI YA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Dar es Salaam.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetakiwa kiuendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la usimamizi wa Utumishi na Maadili ya Walimu nchini ili kuwa na walimu wenye kujituma na wanaozingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao.

Agizo hilo lilitolewa na Naibu Katibu Mkuu (elimu), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Atupele Mwambene tarehe 08 Mei, 2025 kwa niaba ya Waziri wa Nchi wa Ofisi hiyo wakati wa kufunga mafunzo kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC ngazi ya Wilaya na Makao Makuu yaliyofanyika kwa siku nne katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa ni lazima watumishi wa Tume hiyo kuwa na ujuzi wa kutosha katika kusimamia masuala ya walimu ili kuhakikisha walimu wanatoa malezi bora kwa wanafanuzi lengo likiwa ni kuifanya Sekta ya elimu iendelee kuzalisha watoto wanaosaidia Taifa kupiga hatua kimaendeleo.

Hivyo, Naibu Katibu Mkuu huyo aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanazingatia mafunzo waliyopata na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi huku wakizingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo inayohusu majukumu yao.

“Ninawaagiza kila mmoja wenu kuyatumia mafunzo haya kwa ueledi ambao unatakiwa kutoa haki kwa walimu wenye mashauri ya nidhamu na rufaa kwa kufuata Sheria, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Walimu na maadili ya Walimu,” alisema Naibu Katibu Mkuu.

Katika hatua nyingine Bw. Mwambene alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kufanya maboresho mbalimbali katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watumishi wa TSC wanapata ujuzi wa kutosha katika kusimamia utumishi wa walimu

nchini.

“Naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za dhati za kuhakikisha kuwa, Wizara na Taasisi zinazosimamia Utumishi wa Walimu zinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzipatia fedha, nyenzo na watumishi wenye ujuzi na weledi wa kutosha kupitia ufadhili wa Miradi ya Maendeleo ikiwemo mradi wa Uboreshaji Kada ya Ualimu (GPE TSP) ili kuboresha kada ya Ualimu na Sekta ya Elimu Nchini,” alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume ya utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke alisema kuwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikishirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, inatekeleza Programu ya miaka minne (2023/24 hadi 2026/27) ya Uboreshaji wa Kada ya Ualimu (Teacher Support Programme - TSP) ambayo inafadhiliwa na Global Partnership for Education (GPE).

“Tume ya Utumishi wa Walimu ni miongoni mwa Taasisi zinazotekeleza programu hii, ambapo itatekeleza afua zinazosaidia kutoa Motisha na Uwajibikaji kwa walimu (Teachers’ motivation and accountability). Lengo kuu likiwa ni kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ili kuboresha kiwango cha elimu nchini,” alisema Prof. Muruke.

Alifafanua kuwa katika kutekeleza programu hiyo TSC ina jukumu la kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma na Kufanya Mafunzo kwa Watumishi wa Tume kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu.

“Mpaka sasa Tume imeandaa Miongozo hii na kuanza kutoa Mafunzo kwa hatua zaidi za Utekelezaji wa Mradi ambapo Makatibu Wasaidizi 139 kutoka Wilaya zote Tanzania Bara walishafanyiwa mafunzo haya tarehe 4 – 6 Machi, 2025, Tabora kwa awamu ya kwanza. Aidha, Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu nao pia wamefanyiwa mafunzo haya kuanzia



Naibu Katibu Mkuu (elimu), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Atupele Mwambene akitoa hotuba ya kufunga mafunzo ya siku nne kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC tarehe 08 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.

tarehe 23 -25 Aprili, 2025 hapa Dar es Salaam,” alisema Prof. Muruke.

Akitoa neno la utangulizi, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo Maafisa wa Tume ngazi ya Wilaya na Maafisa wa Tume Makao Makuu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Aliongeza kuwa Mafunzo yametolewa kwa kutumia nyenzo shirikishi na mifano halisi, hivyo kuwezesha washiriki kupata uelewa wa kina huku ikitarajiwa kuwa tija itapatikana na ushughulikaji wa mashauri ya nidhamu utazingatia, sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwa haki.

Mwl. Nkwama alihitimisha kwa kuahidi kuwa Tume itaendelea kusimamia jukumu lake la msingi la usimamizi wa Utumishi na Maadili ya Walimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa walimu wanazingatia maadili ya kazi yao.

TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSIMAMIA UTUMISHI NA MAADILI YA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa neno wakati wa hafla ya kufunga mafunzo Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC tarehe 08 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa hafla ya kufunga mafunzo Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC tarehe 08 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akitoa utambulisho wakati wa hafla ya kufunga mafunzo kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC tarehe 08 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.



Baadhi ya walimu ajira mpya wakifutulia mafunzo elekezi kuhusu ajira, haki na wajibu wao hivi karibuni katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSIMAMIA UTUMISHI NA MAADILI YA WALIMU



Washiriki wa mafunzo ya Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC tarehe 08 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam wakiwa katika hafla ya kufunga mafunzo hayo.

Naibu Katibu Mkuu (elimu), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Atupele Mwambene akikabidhi vyeti kwa baadhi ya washiriki wa mafunzo ya siku nne kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu yaliyowahusisha maafisa wa TSC tarehe 08 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania jijini Dar es Salaam.



TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYA YA MULEBA YATOA MAFUNZO KWA WALIMU WA AJIRA MPYA

Na Mwandishi Wetu – Muleba.

Tume ya Utumishi ya Walimu (TSC) Wilaya ya Muleba Mkoani Kagera imetoa mafunzo elekezi kwa jumla ya walimu ajira mpya 167 wa Shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Taarifa hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Muleba, Bw. Avith Mushobozi na kueleza kuwa kati ya walimu hao 127 ni wa Shule za Sekondari na 40 ni walimu wa Shule za Msingi.

Bw. Mushobozi aliwataka Walimu wapya kujua Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma na Utumishi wa Walimu, taratibu za ajira na maendeleo ya Walimu, haki na wajibu kwa walimu, taratibu za mawasiliano na ushughulikiaji wa malalamiko kwa walimu pamoja na maadili na nidhamu kwa walimu.

Mafunzo hayo yalifunguliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Bw. Isaya Mbenje ambapo aliishukuru Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuandaa mafunzo hayo muhimu kwa watumishi wa ajira mpya kazini.

Alisema kuwa baada ya walimu hao kupata mafunzo watakuwa na uelewa mzuri wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia utumishi wa umma kwa ujumla



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Bw. Isaya Mbenje akifungua mafunzo elekezi hivi karibuni kwa walimu wa ajira mpya katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.

husususan katika Utumishi wa walimu.

Bw. Mbenje alisema kuwa kupitia mafunzo hayo walimu watafahamu haki, wajibu na maadili yanayoongoza Utumishi wa umma na taaluma ya kada yao kwa jili ya kuimarisha utendaji kazi na kuongeza kiwango cha ufaulu katika Halmashauri hiyo.

“Tuna changamoto ya kufeli kwa wanafunzi lakini tuna imani kikosi chote hiki kitaleta matumaini ya kuongeza ufaulu, kwa sasa ufaulu ukiwa mdogo sio kwa sababu ya upungufu wa walimu kwani sababu hiyo sasa imetatuliwa,” alisema.

Naye Afisa Elimu Msingi Wilaya

ya Muleba, Mwl. Agasarini Kweka aliwataka walimu hao kufanya kazi kwa moyo, kuwa wabunifu pamoja na kuishi vizuri na jamii.

Alisema kuwa katika maeneo watakayioishi ni lazima kufuata Sheria na Taratibu zilizopo kwenye eneo husika ikiwemo kuhudhuria mikutano ya hadhara na kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii.

Kwa upande wake Afisa Utumishi Wilaya ya Muleba Bw. Christopher Donatus aliwataka walimu hao kujiepusha na changamoto ya kukopa mikopo bila malengo kwani pato likipungua linadhofisha utendaji kazi na hatimaye kushindwa kutekeleza majumu yao kwa weledi.

Baada ya mafunzo hayo Walimu hao walijaza mikataba ya ajira ambapo katika zoezi hilo Kaimu Katibu Msaidizi aliwataka kusoma vizuri mikataba na kuelewa ili waweze kufuata maadili ya kazi yao.

Mafunzo hayo yamehudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Muleba, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) Benki ya NMB, CRDB, Saccos ya Walimu Muleba Mfuko wa Taifa wa BIMA ya afya (NHIF) na Ofisi ya Mdhidhi Ubora wa Shule.



Afisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Muleba Bi. Ester Mkokota akitoa madajuu ya mapambano dhidi ya rushwa wakati wa mafunzo elekezi kwa walimu wapya kazini yaliyofanyika hivi karibuni katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYA YA MULEBA YATOA MAFUNZO KWA WALIMU WA AJIRA MPYA



Baadhi ya Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Muleba, Bw. Theotcus Tito pamoja na Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi ya Walimu Wilaya ya Muleba, Bw. Avith Mushobozi wakifatilia mada za kwenye mafunzo elekezi kwa walimu wapya.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi ya Walimu Wilaya Muleba, Ndugu Avith Mushobozi akitoa mada wakati wa mafunzo elekezi kwa walimu wapya kazini katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba hivi karibuni.



Baadhi ya walimu walioshiriki mafunzo elekezi kwa walimu wapya kazini katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba hivi karibuni.

TSC MVOMERO YATOA KONGOLE KWA RAIS SAMIA KWA KUSIKIA KILIO CHA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Mvomero.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mvomero imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utatuzi wa changamoto zilizokuwa zinawakabili walimu nchini.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mvomero, Bw. Gabriel Mollel wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano (GCU) kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Wilaya hiyo.

Alisema kuwa uongozi wa Awamu ya Sita umeweza kuwapandisha vyeo walimu 2,057 na kuwabadilisha vyeo walimu 201 katika mwaka 2023/2024 na 2024/2025.

Aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeiwezesha Ofisi hiyo usafiri wa pikipiki ambao umerahihisha utoaji wa huduma hasa wanapokwenda kutoa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi

wao.

Bw. Mollel alisema kuwa Ofisi ya Tume kwa Wilaya ya Mvomero imewezeshwa vitendeakazi kama vile kompyuta, printa, mkongo wa mawasiliano TTCL kwa ajili kurahisha upatikanaji na utumaji wa taarifa.

Alisema kuwa Serikali imewezeshwa utoaji wa mafunzo kwa Walimu wakuu na Wajumbe wa Kamati ya Tume kwa ngazi ya Wilaya ya Mvomero hivyo kuwajengea uwezo ambayo yamesaidia kwa kuleta matokea chanya katika kushughulikia mashuari ya kinidhamu kwa walimu.

Bw. Mollel aliongeza kuwa kupitia mafunzo hayo wahusika wamepata ujuzi wa kufanya maamuzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taraibu za Utumishi wa Walimu na Umma kwa ujumla.

Alisema kuwa kupitia mafunzo hayo pia yamewasidia wajumbe kutoa maamuzi sahihi katika Kamati hizo na kufahamu changamoto mbalimbali za walimu na kusaidia kutoa ushauri kwa ofisi namna ya kuzishughulikia

Alisema kuwa kupitia mafunzo kumekuwepo na ushirikiano mzuri kati ya Ofisi za Tume ya Utumishi wa



Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mvomero, Bw. Gabriel Mollel akiwa ofisini kwake hivi karibuni.



Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mvomero, Bw. Gabriel Mollel (aliyekaa) akiwa na Maafisa wenzake mara baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) yaliyofanyika hivi karibuni.

Walimu na Kamati zake na walimu kwa ujumla.

Katika hatua nyingine Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu katika Wilaya ya Mvomero ilifanya ziara shuleni na chuo cha Ualimu ili kueleemisha walimu walioajiriwa na wale walimu tarajali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa walimu wengi hawaingii katika mashauri ya kinidhamu.

Bw. Mollel aliongeza kuwa katika ziara hizo wamekuwa wakitoa ushauri kwa walimu pale ambapo wanapokea malalamiko ili kupunguza utendekaji wa makosa ya kinidhamu.

Bw. Mollel aliongeza kuwa mbinu nyingine wanazotumia kutoa elimu ni kusambaza vipeperushi na kutoa mada zinazohusina na masuala ya maadili, Sheria, Kanuni na Taratibu ili walimu waweze kufahamu taratibu za kazi.

MAAFISA WA TSC WATAKIWA KUWA WALEZI WA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Tabora.

Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya wametakiwa kuwa walezi wa walimu kwa kuwekeza nguvu katika kutoa wa elimu ili kuzuia walimu kutenda makosa ya kinidhamu yanayohatarisha utumishi wao.

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 19 Mei, 2025 mjini Tabora na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke wakati akifungua mafunzo ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume ngazi za Wilaya kutoka mikoa 9 nchini.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa ni muhimu kwa watumishi wa TSC kujenga ukaribu na walimu, kufahamu changamoto zao na kuwaelimisha kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu katika kushughulikia masuala ya kiutumishi.

“Ni muhimu sana kuelewa kwamba kipaumbele cha Tume ni kuhakikisha walimu hawafukuzwi kazi, hatupaswi kukaa kusubiri walimu wakosee ili tuwachukulie hatua za kinidhamu. Hivyo, ni lazima tuongeze nguvu katika kutoa elimu ili walimu wetu wasijikute wanakiuka maadili ya kazi yao, alisema kiongozi huyo.

Prof. Masoud alisisitiza kuwa Ofisi ya Tume ngazi ya Wilaya ikiwa na mashauri mengi ya nidhamu siyo kipimo kwamba inatekeleza majukumu yake vizuri kwa kuwa lengo ni kuhakikisha walimu hawatendi makosa hivyo, inapotokea walimu wanakiuka sana taratibu za kazi ni wazi kuwa Ofisi ya TSC haijatekeleza wajibu wake wa kuwa mlezi kwa walimu kama ilivyokusudiwa.

“Tumieni nguvu kubwa katika kuzuia makosa yasitokee kwa kuziba nyufa badala ya kusubiri kuja kujenga ukuta...msipende kujisifu kwa wingi wa mashauri ya kinidhamu katika maeneo yenu bali mjisifu kwa kuwa walimu wana uelewa wa kutosha juu ya taratibu za utumishi na hivyo hawatendi makosa,” alisema.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akifungua mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.

Aidha, Prof. Muruke aliwataka Maafisa wa Tume wanaohudhuria mafunzo kuzingatia masomo yote ambayo watafundishwa ili kuhakikisha wanatenda haki wakati wa kushughulikia mashauri ya kinidhamu dhidi ya walimu.

Akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza katika maendeleo ya elimu nchini ikiwemo kuiwezesha Tume kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu na Mwongozo wa Mafunzo Elekezi Kwa Walimu Wapya.

“Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa katika maendeleo ya elimu nchini...sisi ni wanufaika na juhudi za Rais kwani katika kipindi chake amepandisha vyeo walimu wote waliokuwa na sifa za kupandishwa. Pia, madai mbalimbali ya walimu yakiwemo malimbikizo ya mishahara, fedha za uhamisho na fedha za likizo yameendelea kulipwa,” alisema.

Aliongeza kuwa hata mafunzo hayo ya siku nne ni matokeo ya juhudi za Serikali za kuwajengea uwezo Maafisa wa Tume ya Utumishi

wa Walimu kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa ili waweze kuongeza ufanisi na weledi katika kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Mwl. Paulina alisema kuwa katika siku nne za mafunzo washiriki watafundishwa masuala muhimu katika utendaji wao wa kazi ambayo ni usimamizi wa nidhamu kwa walimu katika ngazi za shule, utaratibu wa kushughulikia mashauri ya nidhamu kwa walimu, utaratibu na hatua za kushughulikia masuala ya nidhamu yenye jinai, utaratibu na hataua za rufaa kwa ngazi TSC Makao Makuu na kwa Rais.

Alisema kuwa mada nyingine ni menejimenti na utambuzi wa hisia katika kusimamia uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na fafanuzi kuhusu mwongozo wa mafunzo elekezi ya awali kwa walimu wapya.

Mafunzo hayo yanafadhiliwa na Programu ya kuboresha kada ya ualimu (Global Partnership for Education for Education Teachers' Support Profram - GPE TSP) na kuendeshwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania yaliwahusisha Maafisa wa TSC Makao Makuu na wengine kutoka Ofisi za Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Tabora, Kagera, Mara, Simiyu, Geita, Kigoma, Arusha na Njombe.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Mkurugenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Kampasi ya Tabora, Dkt. Joseph Mbwillo akitoa salamu za chuo hicho wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Bi, Apsa Othman akitoa utambulisho wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Lameck Mahewa (kulia) akiwa na Mkurugenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Kampasi ya Tabora, Dkt. Joseph Mbwillo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi nidhamu na rufaa za walimu yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi nidhamu na rufaa za walimu yaliyowahusisha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na washiriki wa mafunzo ya siku nne ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu yaliyowahusisha watumishi wa TSC tarehe 19 Mei, 2025 mkoani Tabora.

PROF. MURUKE ATEMBELEA OFISI YA TSC WILAYA YA TABORA

Na Mwandishi wetu – Tabora.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke ameipongeza Ofisi ya TSC Wilaya ya Tabora kwa kuendelea kutoa elimu kwa walimu jambo linalofanya walimu kuendelea

kutekeleza majukumu yao kwa kuziangatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Ametoa kauli hiyo tarehe 20 Mei, 2025 wakati wa ziara kwenye Ofisi ya Tume Wilaya ya Tabora iliyolenga kupata taarifa ya namna ofisi hiyo inavyotoa huduma kwa walimu.

Pamoja na pongezi hizo, Prof. Muruke amewasisitiza watumishi

wa Tume kuongeza juhudi katika kusimamia maadili ya kazi ya ualimu ili kuhakikisha wanafunzi wanapata malezi katika nyanja zote (kimwili, kiroho, kiakili na kijamii) kama inavyoelekezwa katika Nguzo Kuu za Maadili ya Kazi ya Ualimu.

Baada ya ziara hiyo, Mwenyekiti ameendelea na mafunzo ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume ngazi za Wilaya yanayofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tabora.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akisaini kitabu cha wageni alipowasili katika Ofisi ya TSC Wilaya ya Tabora tarehe 20 Mei, 2025.

SERIKALI YA AWAMU YA SITA YASHUSHA NEEMA KWA WALIMU WA WILAYA YA MOROGORO

Na Mwandishi Wetu – Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya la Morogoro imesema kuwa katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imepandisha vyeo jumla ya walimu 3,268 wa Shule za Msingi na Sekondari katika Wilaya hiyo.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni mjini Morogoro na Kaimu Katibu Msaidizi Bi. Lusubilo Mwaisunga kwenye mahojiano maalumu na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) wa TSC wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa ngazi ya Wilaya.

Alisema kuwa kati ya walimu hao, walimu 2,957 walipandishwa vyeo kwa njia ya kawaida na walimu 311 walipandishwa vyeo kwa njia ya mserekeru.

Bi. Lusubilo alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Rais Samia, Serikali katika Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Morogoro jumla ya walimu 192 wameajiriwa.

Alisema kuwa Serikali imeweza kuweka msawazo wa madaraja kwa walimu walioajiriwa pamoja, walimu wamesaidiwa kuhamishiwa taarifa zao za kiutumishi na mshahara kwenye mfumo kwa walimu waliohama kutoka halmashauri mbalimbali na kufafanua kuwa Serikali imeboresha miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa, mabweni, maabara na ununuzi wa vifaa vya maabara.

Bi. Lusubilo aliongeza kuwa kupitia Kliniki ya Mama Samia imesaidia kutatua kero mbalimbali zinazowakabili walimu ikiwemo madai yaliyo na yasiyo ya mshahara, kupandishwa na kubadilishwa vyeo na kadhalika.

Alisema kuwa Serikali imelipa madeni ya baadhi ya walimu yatokanayo na likizo na wengine wanaendelea kulipwa huku alieleza kuwa madeni yanayotoka na mishahara yameingizwa katika mfumo na kufanyiwa kazi na baadhi yao wamelipwa.

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi alisema kuwa Tume ngazi ya Wilaya ya Morogoro inajivunia uongozi wa awamu ya Sita kwa uwezesaji wa mafunzo kwa Walimu Wakuu ambayo yamewasaidia walimu wakuu kupata uelewa na utaalamu katika ufafanuzi wa kanuni za maaadili na utendaji kazi katika kuwasimamia walimu shuleni.

Aliongeza kuwa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya nidhamu kwa walimu, kwa sababu Wajumbe wa Kamati walipata uelewa jinsi ya kushughulikia na kutenda haki katika utoaji wa maamuzi ya mashauri ya nidhamu ya walimu.

Katika hatua nyingine Kaimu Katibu Msaidizi, Bi. Lusubilo alisema Tume ngazi ya Wilaya ya Morogoro inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu.

Alisema kuwa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Morogoro wanaishukuru Serikali kwa kuwajengea uwezo katika mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za walimu (TSCMIS) na kuwezesha fedha za mafunzo kwa walimu wakuu kuhusu ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Morogoro, Bi. Lusubilo Mwaisunga akiwa ofisini kwake.



Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya Morogoro, Rabia K. Ngaillo, Grace P. Swai na Violet F. Anthony na Elias Kamanga wakiwa katika picha ya pamoja.

**SERIKALI YA AWAMU YA SITA YASHUSHA NEEMA
KWA WALIMU WA WILAYA YA MOROGORO**







WALIMU SHULE YA MSINGI SABASABA B WILAYA YA MOROGORO WAIPONGEZA SERIKALI KWA UTATUZI WA CHANGOMOTO ZAO

Na Mwandishi wetu – Morogoro.

Walimu wa Shule ya Msingi Sabasaba B iliyopo Wilaya ya Morogoro wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa utatuzi wa kero mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili na kuwafanya kuwa na mazingira mazuri ya utoaji elimu kwa wanafunzi.

Wametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa mahojiano na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Morogoro na kutoka Tume Makao Makuu ambapo walieleza kwa Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imewapandisha na kubadishwa vyeo kwa wakati jambo ambalo limeongezea morali katika

kutekeleza majukumu yao.

Mwl. Lilian Mapunda alisema kuwa kupitia Kliniki ya Mama Samia imesaidia kutatua kero mbalimbali zinazowakabili walimu ikiwemo madai yaliyo na yasiyo ya mshahara, kupandishwa na kubadilishwa vyeo.

Mwl. Tulizael Sifuel Kira alisema kuwa Serikali imesaidia kuboresha miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa, mabweni, maabara na ununuzi wa vifaa vya maabara.

Wakati huo huo Walimu hao wameipongeza Ofisi ya Tume Wilaya ya Morogoro kwa kuendelea kutoa elimu ambayo imewasaidia kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Mwl. Lilian alisema kuwa Tume

imekuwa ikitoa elimu juu ya Sheria, Kanuni za utumishi wa walimu na umma kwa ujumla na kusimamia maadili kwa walimu.

Mwl. Tulizael alisema kuwa uwepo wa Tume ya Utumishi wa Walimu umesaidia kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu kwa kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma kwa Walimu na kusimamia maadili kwa walimu.

Mwl. Juma Idrisa Juma alisema kuwa Tume imeendelea kuwatia moyo walimu jambo ambalo linaamsha ari ya utendaji kazi kwa walimu kwa kutatua kero mbalimbali zinazo wakabili walimu ikiwemo ushuri na maelekezo kupitia Ofisi za tume wilayani.

SERIKALI YAPANDISHA VYEO WALIMU 1,274 WILAYANI GAIRO

Na Mwandishi Wetu – Gairo.

Serikali ya Awamu ya Sita imepandisha vyeo jumla ya walimu 1,274 wa Wilaya ya Gairo

katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Gairo, Mwl. Juma Ninkunda wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano (GCU) kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Ofisi ya TSC katika Wilaya hiyo.

Alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Dkt. Samia, Serikali imeajiri na kusajili jumla ya walimu 193 wakiwemo 126 wa Shule za Msigi na 67 wa Sekondari.

“Katika kipindi cha hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan serikali imethibitisha jumla ya walimu 182,” alisema.

Aidha, Mwl. Juma Ninkunda alisema kuwa Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Gairo



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Gairo, Mwl. Juma Ninkunda Eustace akitoa mada kwanye mafunzo yaliyowahusisha wakuu wa shule wote wa shule za msingi za serikali wilayani Gairo chini ya ufadhili wa BOOST.

imeendesha mafunzo kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Kamati ya TSC Wilaya kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma kwa ujumla.

“Tume Wilaya ya Gairo tunatoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa kutoa Mafunzo ambayo yamewasaidia wajumbe wa Kamati za Wilaya kupata uelewa wa kanuni na taratibu za kushughulikia

mashauri ya nidhamu yanayohusu walimu,” alisema.

Aiongeza kuwa mafunzo hayo yamewasaidia wakuu wa shule kupata uelewa na utaalamu

katika ufafanuzi wa Sheria, Kanuni na Taratibu za utendaji kazi katika kuwasimamia walimu shuleni.

Pamoja na hayo, Mwl. Ninkunda alisema kuwa Ofisi yake imekuwa ikifanya ziara katika shule mbalimbali kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa Walimu.

SERIKALI YAPANDISHA VYEO WALIMU 1,274 WILAYANI GAIRO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Gairo, Mwl. Juma Ninkunda Eustace akitoa mada kwanye mafunzo yaliyowahusisha wakuu wa shule wote wa shule za msingi za serikali wilayani Gairo chini ya ufadhili wa BOOST.



Afisa anayeshughulikia masuala ya maadili na nidhamu kwa walimu TSC Gairo Mwl. Amina Iddi Kireti akitoa mada kuhusu vitendo vya ukiukwaji wa maadili kwa walimu wa Shule za Msingi za wakati wa semina kwa wakuu wa shule zote za msingi waliohudhuria kwenye mafunzo yaliyotolewa na ofisi ya TSC Gairo kwa Ufadhili wa BOOST.



Picha ya pamoja kati ya Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na walimu wa Shule ya Msingi Mihongora iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. TSC Wilaya ya Biharamulo ilifanya ziara katika shule hiyo kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu juu ya masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu.



Picha mbalimbali wakati wa Ziara ya Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Biharamulo katika shule ya Sekondari Bizimya na shule za Msingi Kalenge, Kanyoni, Msekwa, Muyovozi, Nyamigere A, Nyamigere B, Rusenge na Rukaragata iliyofanyika tarehe 30 Aprili, 2025.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akifunga Mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa taarifa fupi wakati wa kufunga Mkutano wa Tume hivi karibuni jijini Dodoma.



Makamisha wa Tume ya Utumishi wa Walimu (waliokaa mbele) wakizwa katika hafla ya kufunga Mkutano wa Tume hivi karibuni jijini Dodoma.



Baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Tume wakizwa katika hafla ya kufunga mkutano huo hivi karibuni jijini Dodoma.

MAKAMU MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU AFUNGUA AWAMU YA TANO YA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TSC

Na Mwandishi Wetu – Tabora.

Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Bahati Mgongolwa amefungua awamu ya tano ya mafunzo kwa Watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi yanayofanyika tarehe 26 – 29 Mei, 2025 katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Kampasi ya Tabora.

Katika ufunguzi huo, Bi. Mgongolwa aliwaagiza Watumishi wa Tume kuendelea kutoa elimu kwa walimu ili waweze kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na maadili katika utekelezaji wa majukumu yao.

Bi. Bahati alisema kuwa walimu wakizingatia maadili watasaidia kuandaa wanafunzi bora ambao watakuwa na tija katika maendeleo ya Taifa.

“Ni mara chache kukuta familia ya mwalimu ikiwa katika maadili mabaya lakini mara nyingi familia za walimu zinakuwa na maadili mazuri na sisi kama Tume tunaka walimu waendeleo kuwalea watoto katika maadili mema,” alisema.

Katika hatua nyingine Makamu Mwenyekiti Bi. Bahati aliipongeza Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuendesha mafunzo kwa Watumishi wa Kada Saidizi kwa kuwa watumishi hao ni muhimu kwa maendeleo ya Taasisi yoyote.

“Mimi nawaona Kada Saidi kama viungo katika chakula ...mmefanya jambo muhimu kuendesha mafunzo kwa watumishi hawa kwani itasaidia kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji wao wa kazi kwa manufaa ya Tume katika kuwahudumia walimu,” alisema.

Aliwataka baada ya mafunzo hayo kufanya kazi kwa bidii ili kuifanya Tume kuwa kimbilio la walimu kutokana na huduma bora inayotolewa.

Makamu Mwenyekiti huyo aliwasisitiza washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia maadili ya utumishi



Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Bahati Mgongolwa akifungua awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 26 Mei, 2025 mkoani Tabora.

wa Umma hususan katika suala la kutunza siri katika maeneo wanayofanyia kazi ili kuendelea kulinda hadhi na heshima ya Serikali.

“Nyie Madereva mnapokuwa na viongozi kwenye magari wakati mwingine wanapigiwa simu ya kikazi ni vema maneno mnayosikia yasitoke nje...sio unapotoka unakwenda kuwaeleza watu mazungumzo ya kiongozi wako. Hali kadhalika, Watumishi mnaohusika na utunzaji wa kumbukumbu za ofisi (masijala) na Waandishi Waendesha Ofisi mna nafasi kubwa ya kufahamu mambo mengi ambayo ni siri, jengeni tabia ya kuheshimu maadili ya kazi yenu,” alisema.

Awali Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa mafunzo hayo yanakamilisha kundi la mwisho la Watumishi ambao walikuwa hawajapata mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya misingi ya uadilifu katika utumishi wa umma, misingi ya utoaji wa huduma bora kwa watumishi na wadau na utaratibu

wa utunzaji wa kumbukumbu na uendesaji wa ofisi.

Alisema kuwa mafunzo hayo pia yatawajengea uwezo watumishi hao kuhusu usaidizi kwenye vikao na uandikaji wa taarifa, ushirikiano na mawasiliano kazini, nafasi ya kada saidizi katika mchakato mzima wa uendesaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu.

Aidha, Katibu wa TSC alisema kuwa baada ya Mafunzo kwa watumishi hao mafunzo yanayofuata ni kwa Wajumbe wa Kamati ngazi za Wilaya ambao hawajapata mafunzo hayo kwa kuwa lengo la Tume ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa kuwajengea uwezo watumishi wake.

Mwl. Paulina alisema kuwa mafunzo hayo yanawashirikisha Maafisa wa Tume kutoka Makao Makuu, Wilaya za Mkoa wa Dodoma, Iringa, Katavi, Kilimanjaro, Manyara, Rukwa, Shinyanga na Singida pamoja na Watumishi wa Kada Saidizi kutoka Ofisi za Tume nchi nzima.

**MAKAMU MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU
AFUNGUA AWAMU YA TANO YA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TSC**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 26 Mei, 2025 mkoani Tabora.



Mkurugenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Kampasi ya Tabora, Dkt. Joseph Mbwilo akitoa salamu za chuo hicho wakati wa ufunguzi wa awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 26 Mei, 2025 mkoani Tabora.

Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimaliwa, Bw. Peter Bunyazu akitoa utambulisho wakati wa ufunguzi wa awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 26 Mei, 2025 mkoani Tabora.

MAKAMU MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU AFUNGUA AWAMU YA TANO YA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TSC



Baadhi ya washiriki wakiwa kwenye ufunguzi wa awamu ya tano ya mafunzo kwa watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 26 Mei, 2025 mkoani Tabora.

MAKAMU MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU AFUNGUA AWAMU YA TANO YA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TSC



Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Bahati Mgongolwa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na washiriki wa mafunzo ya watumishi wa Tume yaliyowahusisha Maafisa na Watumishi wa Kada Saidizi tarehe 26 Mei, 2025 mkoani Tabora.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu